BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA KUMI NA MBILI</u>

<u>Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 04 Oktoba, 2023</u>

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. <u>TAARIFA YA SPIKA:</u>

II. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>

Ripoti ya Jitihada za Utekelezaji wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ya mwaka 2022.

<u>Wizara ya Afya:</u>

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Afya kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

<u>Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:</u>

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora,**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 ya Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo; na

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Kwa Ajili ya Kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Afya:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusumamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Jitihada za Utekelezaji wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ya mwaka 2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Afya juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake.

## III. HOJA YA MJUMBE:

**Mhe Yahya Rashid Abdulla**

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu kupongeza uwekezaji wa Bandari ya Malindi Zanzibar.

## IV. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

109. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ni wazi kwa nchi yetu kama zilivyo nchi nyengine hukopa ili kutimiza malengo na mipango yake.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekopwa kwa kipindi hiki cha miaka miwili iliyopita.

(b) Je, kati ya fedha hizo kiasi gani kimewekezwa.

110. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kutokana na mabadiliko ya teknolojia, kumekuwa na ubunifu wa huduma za kifedha kwa njia za Mtandao (E-Banking Service).

Je, ni kwa namna gani teknolojia hii inasaidia kukuza pato la taifa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

103. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hivi karibuni Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) limefanya uchaguzi wa Rais na ndugu Suleiman Mahmoud Jabir amechaguliwa kuwa Rais wa Shirikisho hilo.

(a) Je, Wizara ina mpango gani kwa kushirikiana na uongozi mpya wa ZFF wa kuongeza wigo wa mashindano ya soka kama shindano la "F.A Cup" ili kuchochea hamasa zaidi ya soka kama ile ya mashindano ya "Yamle Yamle Cup".

(b) Je, viongozi wa Wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo, wamepata wasaa wa kukutana na uongozi mpya wa ZFF ili kubainisha njia za utekelezaji wa mikakati ya kukuza soka la Zanzibar.

104. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kutokana na juhudi kubwa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Zanzibar imekuwa ikizalisha vipaji vingi vya michezo hasa kwenye soka na kupata soko la ajira nje ya nchi.

(a) Katika kuhakikisha vijana wetu hao wanalindwa na wanapata maslahi bora na mazuri, je, Serikali imeweka utaratibu upi wa kuwapatia huduma ya kisheria vijana wetu hao, pale wanapofunga mikataba na timu zinazowanunua.

(b) Je, Viongozi wa Shirikisho la Mpira la Zanzibar (ZFF) wanayo "data base" ya kujua idadi ya wachezaji kutoka Zanzibar wanaocheza soka la kulipwa na hali ya mikataba yao.

(c) Je, wakati inapotokea changamoto ya kimkataba baina ya mchezaji na timu yake, hatua gani zinachukuliwa na ZFF au Wizara kutoa usaidizi pale inapohitajika kwa mchezaji ili kulinda kipaji na ajira yake.

**Wizara ya Afya:**

58. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kuzipambania huduma za afya kutolewa kwa kiwango kilicho bora zaidi nchini, bado tunakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na wizi wa madawa ya Serikali kuibwa na kuuzwa katika maduka ya dawa ya watu binafsi.

(a) Je, Wizara yako inachukua hatua zipi za kuwadhibiti madaktari wasiokua wazalendo ambao huchukua dawa za Serikali na kuziuza kupitia maduka yao binafsi (Pharmacy).

(b) Ni madaktari na watumishi wengine wangapi wameshapatikana na hatia hiyo.

(c) Je, ni hatua zipi za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya madaktari na watendaji wengine waliohusika na wizi huo, ili iwe fundisho kwa wengine.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

98. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la ajali zinazopelekea vifo na majeruhi ambazo nyingi kati ya hizo husababishwa na madereva wazembe.

(a) Katika kukabilana na hali hiyo, Je, Serikali ipo tayari kuirekebisha Sheria ya Usafiri Barabarani na kuweka masharti kuwa dereva yeyote atakayesababisha ajali kwa uzembe, pamoja na adhabu nyengine, afungiwe leseni yake kwa muda wa miezi 12 au zaidi.

(b) Je, Serikali ipo tayari kuirekebisha Sheria ya Usafiri Barabarani kwa kuweka masharti ya kuwafutia leseni kwa muda wa zaidi ya miezi 6 madereva watakaobainika kuendesha vyombo barabarani wakiwa wametumia kilevi chochote.

(c) Je, ni lini Serikali italeta kipimo maalumu cha kuwabaini madereva wanaotumia kilevi (breathalyzer) wakati wa kuendesha vyombo vya moto ili kudhibiti ajali za kizembe nchini.

102. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu sasa njia za ndani za Rahaleo kutoka barabara kuu kuelekea kituo cha Afya cha Rahaleo karibu na Studio na njia ya kutoka barabara kuu kuelekea ZBC-Redio, zimekuwa katika hali mbaya na kusababisha usumbufu kwa wananchi hasa katika kipindi cha mvua.

(a) Je, hatua gani za haraka zitachukuliwa kuzijenga njia hizo.

(b) Je, ni lini ukarabati wa kudumu wa njia hizo utafanyika badala ya kuwekwa kifusi ambacho kinapotea wakati wa mvua.

## V. TAARIFA YA SERIKALI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ripoti ya Jitihada za Utekelezaji wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ya mwaka 2022.

## VI. HOJA ZA SERIKALI:

### Wizara ya Afya:

Ripoti ya Wizara ya Afya kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2022/2023.

### Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:

Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake – Kusomwa kwa mara ya Pili.

## VII. HOJA YA MJUMBE:

### Mhe. Yahya Rashid Abdulla

Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu kupongeza uwekezaji wa Bandari ya Malindi Zanzibar.

## VIII. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora,**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nam. 11 ya 2003 ya Kutunga Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mahakama ya Kadhi Nam. 9 ya 2017 na Kutunga Sheria ya Mahakama za Kadhi na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha Kwa Ajili ya Kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa wa mara ya Kwanza.

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar na Kuweka Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Waziri wa Afya:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kwa ajili ya Ununuzi, Utengenezaji, Uhifadhi na Usambazaji wa Dawa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

**Zanzibar,** (Raya Issa Msellem)
**04 Oktoba, 2023.** **KATIBU WA BARAZA.**